# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

## MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU WA ELIMU YA AWALI

## NGAZI YA CHETI

## VITENDO VYA MASOMO

**2009**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 2009

ISBN ............................................

Haki zote zimehifadhiwa.  Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Muhtasari huu umebuniwa na kutayarishwa na:

Taasisi ya Elimu Tanzania
P. O. Box 35094
Dar-es-Salaam
Tanzania

Tel: +255 222 773006, 2774420
Fax: +255 222 774420
Tovuti: director.tie@tie.go.tz

## TAMKO LA IDHINI

Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za awali. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya cheti miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha .

Andiko hili linatambuliwa kuwa ni **Muhtasari wa Vitendo vya Masomo Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali Ngazi ya Cheti** wa mwaka 2009

Imeidhinishwa na …………………………………….

Sahihi…………………………………………………

Tarehe……………………………………… 2009

Kamishna wa Elimu

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

S. L. P. 9121

Dar-es-Salaam

Simu: +255 222 110150, 110179, 11046

Nukushi: +255 222 113271

Tovuti: www.moe.go.tz

## YALIYOMO

**Ukurasa**

**UTANGULIZI**………………………………………………………… 3
Maelezo kuhusu muhtasari........................................................................ 3
Madhumuni ya Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali Ngazi ya Cheti.....5
Ujuzi wa Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali Ngazi ya Cheti...............5
Malengo ya Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali Ngazi ya Cheti..........6
Muundo wa muhtasari..........................................................................6
Upimaji na tathmini.................. ........................................................7
Muda wa Mafunzo..................................................................................7

**MAUDHUI YA VITENDO VYA MASOMO.........................................9**
Ujuzi wa somo………………………………………………………… 10
Malengo ya somo……………………………………………………… 10
Vitendo vya Kujifunza Kiswahili…...……………………………………..10
English Learning Activities…...............…………………………………..23
Vitendo vya Kujifunza Sayansi…………...………………………………..39
Vitendo vya Kujifunza Hisabati...…………………………………………55
Vitendo vya Kujifunza Haiba na Michezo………..……………………….82
Vitendo vya Kujifunza Sanaa……...………………………………………92

## UTANGULIZI

### Maelezo kuhusu Muhtasari

Muhtasari huu wa Ualimu wa Elimu ya Awali Ngazi ya Cheti, kwa ajili ya Vitendo vya Masomo ya Elimu ya Awali umeboreshwa kutokana na marekebisho ya Muhtasari wa Elimu ya Awali wa mwaka 2005. Mabadiliko hayo ya ufundishaji yamezingatia mtazamo wa kumjali mwanafunzi na kumshirikisha katika shughuli zote za ufundishaji na ujifunzaji. Katika mtazamo huo, mwalimu huwa mwezeshaji na mwanafunzi hujifunza kwa kutenda kwa kutumia uzoefu wake na kujitafutia maarifa kwa kushirikiana na wengine. Huu ni muhamo wa ruwaza kutoka mfumo ambao mwalimu ndiye mtendaji mkuu kwenda kwenye mfumo ambao mwanafunzi ndiye mtendaji mkuu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.

Muhtasari huu pia umeboreshwa kwa kuzingatia mahitaji na mabadiliko yanayotokea katika jamii, masuala mtambuko na malengo ya milenia kwa kuzingatia falsafa ya Elimu ya Kujitegemea. Ufundishaji pia umezingatia vipengele muhimu vinavyotokana na nadharia mbalimbali za elimu ya awali duniani zinazokubaliana na falsafa hiyo.

Katika ufundishaji na ujifunzaji wa vitendo vya masomo inasisitizwa kwamba misingi ifuatayo izingatiwe:

1. Ufundishaji kwa vitendo unaomjali mtoto
2. Ujifunzaji unaomwelekeza mtoto kukabili changamoto zilizo katika mazingira yake
3. Ufundishaji unaojali utayari wa mtoto katika kujifunza
4. Uwepo wa ulinzi na usalama wa mtoto katika mazingira ya ujifunzaji
5. Ujifunzaji unaolingana na mahitaji ya mtoto
6. Ujifunzaji unaolenga kujenga na kukuza udadisi katika maisha ya kila siku
7. Ufundishaji unaozingatia tathmini inayokwenda sanjari na ujifunzaji wa mtoto.

Mkufunzi wa somo hili anashauriwa kutumia mbinu zilizopendekezwa katika muhtasari na nyingine ambazo zinalenga kufanya mwanachuo ajifunze zaidi. Baadhi ya mbinu hizo

ni kama onesho mbinu, maigizo, nyimbo, michezo, mtandao, maswali na majibu, nyota za maneno, kufikiri zaidi na majadiliano katika vikundi. Pia anashauriwa kuwa mbunifu wa kutengeneza na kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yake.

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni kurasa za mwanzo za muhtasari na sehemu ya pili ni maudhui ya Elimu ya Awali. Kurasa za mwanzo za muhtasari zimejumuisha:- Jalada, Haki Miliki, Yaliyomo na Utangulizi ambao umehusisha Usuli, Muda wa Mafunzo, Madhumuni, Ujuzi na Malengo ya Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali Ngazi ya Cheti na Muundo wa Muhtasari.

Sehemu ya maudhui imejumuisha Vitendo sita (6) vya Masomo ambavyo ni:

- Vitendo vya kujifunza Kiswahili
- English Learning Activities
- Vitendo vya kujifunza Hisabati
- Vitendo vya kujifunza Sayansi
- Vitendo vya kujifunza Haiba na Michezo
- Vitendo vya kujifunza Sanaa

Vipengele vya Vitendo vya kila somo vinajumuisha Ujuzi, Malengo, Mada Ndogo, Muda, Malengo Mahsusi, Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia, Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia, Upimaji na Rejea. Pia, mwanachuo atatakiwa kusoma maudhui ya taaluma za masomo yaliyoko katika mihtasari ya Ualimu, Elimu ya Msingi.

**Upimaji na Tathmini**

Mwanachuo atafanyiwa upimaji katika ufuatiliaji wa maendeleo yake kwa kila somo atakalosoma wakati wa mafunzo yake. Upimaji huo utakuwa wa aina mbili: upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu (tathmini endelevu) utakuwa na jumla ya 50% ya alama zote kabla ya kuhitimu, ambapo upimaji tamati (tathmimi tamati) ambao ni mtihani wa mwisho utachukua alama 50% zilizobaki. Vipengele vitakavyofanyiwa upimaji ni taaluma na ufundishaji. Njia za upimaji zinatofautiana na zinaoneshwa kwa

kila vitendo vya somo husika. Mfano wa njia hizo ni; majaribio, kazi mradi, kazi binafsi, mtihani wa muhula, utafiti na mtihani wa mwisho (taaluma na ufundishaji). Matokeo ya upimaji wa mafunzo yote yatatolewa baada ya mwanachuo kumaliza mwaka wa pili.

**Muda wa Mafunzo**

Muda wa mafunzo ni miaka miwili ambapo mwanachuo atasoma darasani siku 194 ambazo ni wiki 32 katika kila mwaka. Katika kila mwaka kutakuwa na wiki 20 za muhula wa kwanza na wiki 12 za muhula wa pili. Wiki 16 zitatumika kwa maandalizi na mazoezi ya kufundisha ya muda mrefu (BTP), wiki 8 kwa mwaka wa kwanza na wiki 8 kwa mwaka wa pili. Kila wiki itakuwa na siku 5 za masomo na vipindi 6. Kila kipindi ni saa 1.

# VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI

**Ujuzi**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili ya Vitendo vya Kujifunza Kiswahili ngazi ya cheti, mwanachuo atakuwa amepata ujuzi wa:-

1. Kutumia lugha inayojenga na kukuza maadili yanayofaa kwa watoto kwa mujibu wa jamii husika
2. Kubuni mbinu mbalimbali za kuwafundisha watoto stadi za awali za kusoma na kuandika
3. Kuwashirikisha watoto katika vitendo mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia lugha ya Kiswahili.

**Malengo**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili ya Ualimu wa Elimu ya Awali ngazi ya Cheti, mwanachuo anatarajiwa aweze:-

1. Kuwawezesha watoto kujenga stadi sahihi za mawasiliano kulingana na umri wao
2. Kuwaelekeza watoto kutumia lugha inayofaa katika kujenga mahusiano mema
3. Kutumia ubunifu utakaowawezesha watoto kujifunza kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

**Tathmini**

Vitendo vya Kujifunzia Kiswahili vitatumia tathmini endelevu na tamati katika ufuatiliaji na upimaji wa maendeleo ya mwanachuo wakati wa mafunzo yake. Upimaji endelevu (tathmini endelevu) utakuwa na jumla ya 50% ya alama zote kabla ya kuhitimu, ambapo mtihani wa mwisho (tathmini tamati) utachukua 50% zilizobaki. Ufupisho wa upimaji huo ni kama unavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la Upimaji Endelevu na Tamati**

| Vipengele | Mbinu za Upimaji | Mwaka wa Kwanza | | Mwaka wa Pili | | Idadi | Alama |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Muhula wa kwanza** | **Muhula wa Pili** | **Muhula wa kwanza** | **Muhula wa Pili** | | |
| **Taaluma** | Majaribio | 1 | 1 | | | 2 | 3 |
| | Kazi mradi | 1 | 1 | | | 2 | 5 |
| | Mtihani wa mwisho | 1 | 1 | | | 2 | 2 |
| **Ufundishaji** | Majaribio | 1 | 1 | | | 2 | 3 |
| | Mkoba wa Kazi | 1 | 1 | | | | 2.5 |
| | Kazi mradi | 1 | 1 | | | 2 | 2 |
| | Ufundishaji kiduchu | 1 | 1 | | | | 2.5 |
| **Mtihani wa mwisho wa muhula** | Taaluma na Ufundishaji | 1 | 1 | | | 2 | 15 |
| **Mazoezi ya Kufundisha** | 1. Maandalizi ya Ufundishaji<br>2.Ufundishaji darasani | | 1 | | | 1 | 5 |
| **Mazoezi ya muda mrefu** | 1.Fomu za uchunguzi<br>2.Ufaraguzi wa zana<br>3.Mkoba wa Kazi | | | 1 | | | 10 |
| **Jumla ya Alama za Upimaji Endelezi** | | | | | | | **50** |
| **Mtihani wa Baraza la Mtihani wa Taifa** | | | | 1 | | | **50** |
| **Jumla Alama za Upimaji Endelezi na Tamati** | | | | | | | **100** |

**NB-**

i) Mazoezi ya darasani jumla ya alama ni alama 20
BTP alama 5
Mitihani ya Mihula (miwili) alama 15
Mazoezi ya kufundisha muda mrefu 10

## 1.0 UKUAJI WA MTOTO KATIKA KUJIFUNZA LUGHA

### 1.1 Hatua za Ukuaji katika kujifunza lugha

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza hatua za ukuaji wa lugha kwa mtoto katika umri wa miaka 0-6
b) Kufafanua mazingira yanayomfanya mtoto ajieleze
c) Kubainisha mbinu na zana za kufundishia hatua za ukuaji wa lugha kwa mtoto
d) Kuandaa andalio la somo la hatua za ukuaji wa lugha kwa mtoto
e) Kufundisha hatua za ukuaji wa lugha kwa mtoto

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Bungua bongo
ii) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji
iii) Intaneti
iv) Mazoezi ya kufundisha

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

i) Hadithi fupi fupi
ii) Picha za aina mbalimbali
iii) Nyimbo za watoto
iv) Kompyuta na intaneti

**Upimaji**

i) Maribio
ii) Insha
iii) Orodha hakiki

## 2.0 STADI ZA KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### 2.1 Kujifunza Kusikiliza

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kusikiliza
b) Kubainisha mbinu atakazotumia kumfundisha mtoto kuwa msikivu
c) Kuandaa somo kuhusu kusikiliza
d) Ufundishaji kiduchu kuhusu kusikiliza
e) Kufanya tathmini ya ufundishaji kiduchu

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Majadiliano
ii) Fikiri, jozisha shirikisha
iii) Igizo
iv) Ufundishaji kiduchu

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

i) Nyimbo
ii) Redio na redio kaseti
iii) Kengele
iv) Vifaa vingine vinavyotoa sauti mbalimbali
v) Luninga na intaneti

**Upimaji**

i) Chemsha bongo
ii) Insha
iii) Fomu ya uchunguzi

### 2.2 Kujifunza Kuitikia

**Muda:** Saa 9

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua mambo yanayoweza kuwezesha au kukwamisha mwitikio wa mtoto

b) Kuchambua mbinu mbalimbali za kumfundisha mtoto kuitikia

c) Kuandaa somo kuhusu mada ndogo ya kuitikia

d) Kufanya mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja katika shule kuhusu kuitikia

e) Kufanya tathmini ya ufundishaji na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Maswali na majibu

ii) Fikiri jozisha shirikisha

iii) Majadiliano

iv) Mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja shule jirani

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

i) Picha zinazoonesha mazingira yanayokwamisha usikivu

**Upimaji**

i) Majaribio

ii) Fomu ya uchunguzi

iii) Orodha hakiki

## 2.3 Kujifunza Kutamka Herufi, Maneno na Sentensi

**Muda:** Saa 10

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua mbinu za kumfundisha mtoto matamshi

b) Kuchambua mambo mbalimbali yanayosababisha makosa ya matamshi kwa mtoto na mbinu za kusahihisha makosa hayo

c) Kujadili umuhimu wa kusahihisha makosa ya matamshi

d) Kufanya somo la mfano kuhusu matamshi ya herufi, maneno na sentensi

e) Kufanya tathmini ya ufundishaji

**Mbinu za Kujifundishia na Kujifunzia**

i) Bungua bongo

ii) Maswali na majibu

iii) Onesho mbinu

iv) Majadiliano

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

i) Chati zenye herufi, maneno na sentensi fupi

ii) Vifani vya herufi

**Upimaji**

i) Majaribio

ii) Orodha kaguzi

## 2.4 Kujifunza Kuwasiliana

**Muda:** Saa 8

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha na kufafanua umuhimu wa kumwezesha mtoto kutumia lugha inayojenga mahusiano mazuri katika jamii

b) Kueleza mbinu za kumwezesha mtoto kuwasiliana kwa kutumia lugha ya heshima katika miktadha mbalimbali.

c) kuandaa somo kuhusu kuwasiliana

d) Ufundishaji rika kuhusu kusikiliza

e) Kufanya tathmini ya ufundishaji

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Maswali na majibu

ii) Majadiliano
iii) Ufundishaji rika

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

i) Intanet, luninga na kaseti za video
ii) Picha zinazoonesha watu wakiwasiliana

**Upimaji**

i) Mazoezi
ii) Fomu ya uchunguzi

**2.5 Kujifunza Kusimulia**

**Muda:** Saa 9

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kujadili mambo ya kuzingatia katika kumwezesha mtoto kusimulia
b) Kufafanua mbinu za kumfundisha mtoto kusimulia kwa ufasaha na umuhimu wake
c) Kuandaa somo kuhusu kusimulia
d) Kufundisha somo la mfano kuhusu kusimulia
e) Kufanya tathmini ya ufundishaji

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Bungua bongo
ii) Majadiliano
iii) Onesho mbinu la jinsi ya kusimulia kwa ufasaha
iv) Mazoezi ya kufundisha

**Zana/Vifaa vya Kufundishia**

i) Hadithi fupi fupi
ii) Picha za aina mbalimbali

**Upimaji**

(i) Majaribio

(ii) Insha

(iii) Orodha kaguzi

## 3.0 STADI ZA AWALI ZA KUSOMA

### 3.1 Maandalizi ya Kusoma

**Muda:** Saa 9

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha mazingira vutivu ya kusoma na umuhimu wa mtoto kufahamu majina ya vitu na watu katika mazingira yake

b) Kuchambua mbinu na zana/vifaa anuai vya kumwezesha mtoto kufahamu majina ya vitu na watu mbalimbali katika mazingira yake.

c) Kuandaa andalio la somo kuhusu kusoma

d) Kufanya mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja kusoma katika shule

e) Kufanya tathmini ya ufundishaji

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Majadiliano ya vikundi

ii) Bungua bongo

iii) Fikiri, jozisha shirikisha

iv) Mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

i) Picha za watu na vitu

ii) luninga na kanda za video

iii) Intaneti

**Upimaji**

(i) Insha
(ii) Jaribio
(iii) Orodha hakiki

## 3.2 Kujifunza Kutambua Herufi, Silabi, Maneno na Sentensi

**Muda:** Saa 12

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza jinsi mtoto anavyoonesha utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi fupi na rahisi
b) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kumwelekeza mtoto kusoma herufi, silabi, maneno na sentensi fupi na rahisi
c) Kufafanua makosa yanayoweza kutokea mtoto anapojifunza kusoma, mbinu na umuhimu wa kurekebisha makosa hayo
d) Kufanya somo kuhusu utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi fupi na rahisi
e) Kufanya ufundishaji rika wa herufi, silabi, maneno na sentensi fupi na rahisi

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Onesho mbinu
ii) Majadiliano
iii) Kuigiza

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Vioo
ii) Kadi za maneno, silabi, herufi, sentensi
iii) Picha za vitu na watu mbalimbali.

**Upimaji**

i) Majaribio

ii) Maswali ya mdomo

iii) Orodha hakiki

## 4.0 STADI ZA AWALI ZA KUANDIKA

### 4.1 Maandalizi ya Kujifunza Kuandika

**Muda**: Saa 26

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kujadili mambo ya kuzingatia katika kuwaandaa watoto kujifunza kuandika

b) Kubainisha makosa ya watoto katika kujifunza kuandika, mbinu na umuhimu wa kurekebisha makosa hayo

d) Kuzainisha mbinu na zana za kufundishia maandalizi ya kujifunza kuandika

e) Kuandaa andalio la somo kuhusu maandalizi ya kujifunza kuandika

e) Kufundisha kuandika kwa kutumia mbinu mbalimbali

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Maswali na majibu

ii) Majadiliano

iii) Fikiri jozisha shirikisha

iv) Mazoezi ya kufundisha

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Vitu halisi/Picha

ii) Vifani vya herufi

iii) Kadi za mkwaruzo

**Upimaji**

i) Orodha hakiki

ii) Insha

iii) Majaribio

**REJEA**

1. Bruce, T. (Ed) (2006). Early Childhood. A Guide for Students
Stadi za Awali za Kujifunza Kusoma.

2. Brunner, J. (1960). *The Process of Education*. Cambridge: Harvard University Press.

# ENGLISH LEARNING ACTIVITIES

**Competences**

By the end of the two-year pre-primary teacher education certificate course, the student teacher should have the ability in:

1. Using knowledge and skills for facilitating development of appropriate norms and values through English language
2. Facilitating children's ability to express themselves in their day-to-day life
3. Using creativity in facilitating children's ability to read and write
4. Involving children actively in different English learning activities.

**Objectives**

By the end of the two-year pre-primary teacher education certificate course, the student teacher should be able to:

1. Facilitate children to develop language skills appropriate to their level
2. Guide children in using polite and appropriate language in their day-to-day life activities
3. Engage children in English learning activities leading to development of self-expression skills.

**Assessment**

English Language Learning Activities will use both formative and summative evaluation to monitor and assess each student teacher's progress in his or her training. Continuous assessment (formative evaluation) shall constitute 50% of the total marks before graduation similar to the final examination (summative evaluation) which shall constitute 50%. The aspects to be assessed on continuous and summative basis are summarized in the table below:

**Jedwali la Upimaji Endelevu na Tamati**

| **Item** | **Assessment tools** | **First Year** | | **Second Year** | **Frequence** | **Marks %** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **First Term** | **Second Term** | | | |
| **Academic** | Test | 1 | 1 | | 2 | 3 |
| | Project | 1 | 1 | | 2 | 5 |
| | Individual assignment | 1 | 1 | | 2 | 2 |
| **Pedagogy** | Test | 1 | 1 | | 2 | 3 |
| | Practicals | 1 | 1 | | | 2.5 |
| | Essay writing | 1 | 1 | | 2 | 2 |
| **Terminal examination** | Academic and Pedagogy | 1 | 1 | | 2 | 15 |
| **Block Teaching Practice (BTP** | Preparation for teaching Microteaching | - | 1 | | 1 | 5 |
| **Field Attachment** | Observation form Improvisation of T/L materials Portfolio | | | 1 | | 10 |
| **Total scores for continuous assessment** | | | | | | **50** |
| **Final Examination (academic and pedagogy)** | | | | 1 | | **50** |
| **Total score for continuous and summative assessment** | | | | | | **100** |

**NB-**

i) Class exersises 20
BTP 5
Terminal examination for two terms 15
Teaching practice 10

## 1.0 CHILD DEVELOPMENT IN FOREIGN LANGUAGE LEARNING

### 1.1 Language Development

**Time:** 6 hours

**Specific Objectives**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:

a) Explain how to identify each child's English language ability at entry to pre-primary school and its importance

b) Discuss environments that facilitate a child to express himself or herself well in English.

c) Elaborate strategies of identifying children's English language ability with respect to speaking, reading and writing

d) Prepare a lesson plan on language development

e) Demostrate language development lesson, evaluate and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

i) Brainstorming

ii) Group discussion and plenary presentation

iii) Demonstration

**Teaching and Learning Resources**

(i) Cards with alphabets, words, short sentences

(ii) Songs

**Assessment**

(i) Essay

(ii) Test

## 2.0 LISTENING AND SPEAKING SKILLS

### 2.1 Learning to Listen

**Time:** 14 hours

**Specific Objectives**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:-

a) Explain factors to be considered for effective listening
b) Discuss different strategies of assessing each child's ability to listen
c) Analyse different techniques for teaching young children to listen
d) Demostrate peer teaching on listening
e) Reflect on the lesson taught and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

(i) Brainstorming
(ii) Think pair share
(iii) Group discussions and plenary session
(iv) Peer teaching

**Teaching and Learning Resources**

(i) Real objects
(ii) Audio visual aids
(iii) Radio
(iv) Internet

**Assessment**

(i) Quiz
(ii) Essay

### 2.2 Learning to Respond

**Time:** 6 hours

**Specific Objectives**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:-

a) Explain various ways that demonstrate each child's understanding from listening
b) Analyse factors that hinder the child's ability to respond to listening

c) Explain techniques for assessing each child's ability to respond and those which facilitate child's response to listening
d) Perform microteaching lesson on responseto listening
e) Evaluate the demonstrated lesson and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

(i) Group discussions and plenary session
(ii) Think pair share
(iii) Drill and practice
(iv) Demonstration

**Teaching and Learning Resources**

(i) Audio and visual CD's
(ii) Audio-visual materials (video)
(iii) Pictures/diagrams of people talking and listening

**Assessment**

i) Essay
ii) Observation checklist

### 2.3 Pronunciation of Letters and Words

**Time:** 13 hours

**Specific Objectives**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:-

a) Explain techniques used in the assessment of each child's ability to pronounce letters and words and techniques for teaching speaking
b) Identify different factors that cause speech problems, techniques of correcting speech errors and importance of proper pronunciation of words
c) Prepare a lesson plan to teach pronunciation of letters and words
d) Perform Single Lesson Teaching Practice to a nearby school
e) Evaluate the lesson taught and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

(i) Library and internet search

(ii) Group discussion and plenary presentation

(iii) Think pair share

(iv) Single Lesson Teaching Practice

**Teaching and Learning Resources**

(i) Reference books

(ii) Audio, visual and audio visual aids

(iii) Internet

**Assessment**

(i) Essay

(ii) Observation checklist

(iii) Quiz

## 2.4 Learning to Communicate

**Time:** 9 hours

**Specific Objectives:**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:-

a) Explain techniques used to assess each child's ability to use language politely and appropriately and the importance of using polite and appropriate language

b) Describe the environment that sustain conversation and factors that hinder communication

c) Prepare a lesson on learning to communicate

d) Perform demostration on prepared lesson

e) Evaluate the lesson taught and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

i) Discussion

ii) Brainstorming

iii) Demonstration

iv) Think pair share

**Teaching and Learning Resources**

(i) Internet

(ii) Real objects

(iii) Audio, visual and audio visual aids

**Assessment**

i) Essay

ii) Test

iii) Observation checklist

## 2.5 Narration

**Time:** 9 hours

**Specific Objectives:**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:-

a) Explain the concept of narration and events that a child can narrate

b) Analyse various techniques of assessing each child's ability to narrate

c) Discuss factors that facilitate a child to narrate and techniques used for teaching children to narrate

d) Prepare a lesson on narration

e) Conduct peer teaching on narration, evaluate the lesson and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

(i) Brainstorming

(ii) Discussion

(iii) Peer teaching

**Teaching and Learning Resources**

(i) Real objects

(ii) Puppets/cartoons

(iii) Pictures/diagrams

(iv) Audio, visual and audio-visual aids

**Assessment**

(i) Quiz

(ii) Test

(iii) Observation checklist

## 3.0 PRE-READING SKILLS

### 3.1 Preparations for Reading

**Time:** 9 hours

**Specific Objectives**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:-

a) Identify the environment that arouses children's interest in reading and various strategies for assessing each child's readiness to read.
b) Explain the importance of knowing names of objects, animals and people as prerequisites for learning to read
c) Identify techniques and teaching aids for teaching children names of objects, animals and people and their relationships
d) Prepare a lesson on preparation for reading
e) Conduct micro teaching, evaluate the lesson and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

(i) Think-pair-share

(ii) Discussion

(iii) Questions and answers

(iv) Micro teaching

**Teaching and Learning Resources**

(i) Pictures of different things

(ii) Printed materials

(iii) Cartoons

(iv) Internet facilities

(v) Alphabet, word and short sentences cards

**Assessment**

(i) Essay

(ii) Test

(iii) Observation checklist

## 3.2 Reading Letters, Syllables, Words and Sentences

**Time:** 15 hours

**Specific Objectives**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:-

a) Identify various methods of assessing each child's ability to read letters, syllables, words and short sentences and techniques tha t facilitate reading

b) Discuss techniques for correcting reading errors and its importance

c) Prepare a lesson plan on reading of letters, syllables, words and sentences

d) Perform a Single Lesson Teaching Practice on the lesson prepared

e) Evaluate the lesson taught and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

(i) Brainstorming

(ii) Group discussion

(iii) Think pair share

(iv) Single Lesson Teaching Practice

**Teaching and Learning Resource**

(i) Action and puzzle cards

(ii) Reading folders

(iii) Sand paper letters/alphabet

(iv) Movable alphabet

**Assessment**

(i) Exercise

(ii) Quiz

(iii)Observation checklist

## 4.0 PRE-WRITING SKILLS

### 4.1 Preparing Children to Learn Writing

**Time:** 15 hours

**Specific Objectives**

At the end of this sub-topic a student teacher should be able to:-

a) Explain different techniques for assessing each child's ability in writing and techniques that facilitate a child to write

b) Discuss factors to be considered in preparing a child to learn writing

c) Discuss the techniques used for correcting writing errors and its importance

d) Prepare a lesson on preparing children to learn writing

e) Demonstrate the prepared lesson, evaluate and provide feedback

**Teaching and Learning Strategies**

(i) Brainstorming

(ii) Discussion

(iii) Demonstration

**Teaching and Learning Resources**

(i) Sand letters

(ii) Letter cards

(iii) Movable alphabets

(iv) Small chalkboards

**Assessment**

(i) Essay

(ii) Test

(iii) Observation checklist

**Bibliography**


1. Bruner, J. (1960). *The Process of Education*. Cambridge: Harvard University Press.
2. Gimson, A.C. (1990). *An Introduction to the Pronunciation of English* (4th ed). London & New York: Edward Arnold.
3. Holt, N. (2007). *Bringing the High/Scope Approach to Your Early Years Practice*. London & New York: Routledge.
4. Isaacs, B. (2007). *Bringing the Montessori Approach to Your Early Years Practice*. London & New York: Routledge.
5. Nicol, J. (2007). *Bringing the Steiner Waldorf Approach to Your Early Years Practice*. London & New York: Routledge.
6. O'Connor, J.D. (1967). *Better English Pronunciation*. London: Cambridge University Press.
7. Thornton, L & Brunton, P. (2005). *Understanding the Reggio Emilia Approach*. London: David Fulton.
8. http://www.childdevelopmnet inf.com/development/language – development.shtml
9. http://www2.scholastic.com/browse/article.jsp?id=1503

10. http://sensory-processing-disorder.com/pre-writing-activities-for-preschool-children.html

# VITENDO VYA KUJIFUNZA HISABATI

**UJUZI**

Baada ya miaka miwili mwanachuo anatarajiwa kuwa na ujuzi wa:

1. Kutumia stadi za kumuelekeza mtoto jinsi ya kuongeza na kupunguza vitu
2. Kutumia stadi mbalimbali za vitendo vya Hisabati katika kumuelekeza mtoto jinsi ya kutambua kutathmini na kutunza fedha.
3. Kutumia stadi za vipimo katika maeneo mbalimbali.

**MALENGO**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili, mwanachuo aweze:

1. Kuandaa na kumwezesha ujifunzaji wa mtoto kwa kutumia matendo rahisi ya hesabu.
2. Kutumia stadi za kuwezesha mtoto kutambua aina mbalimbali za fedha, matumizi na utunzaji wa fedha.
3. Kupanga, kuendeleza na kuwezesha ujifunzaji wa stadi mbalimbali za vipimo katika elimu ya awali.

**UPIMAJI NA TATHMINI**

Mwanachuo atapimwa kwa mazoezi ya darasani, majaribio, projekti, ufundishaji wa mazoezi (vitendo), mitihani ya mihula na mtihani wa mwisho.

Mtihani wa mwisho utakuwa na uzito wa 50%. Vipengele vingine vitakuwa na uzito wa jumla ya 50% kwa mtawanyo kama unavyoonenkana katika jedwali liufuatalo:

**Jedwali la Upimaji Endelevu na Tamati**

| Vipengele | Mbinu za Upimaji | Mwaka wa Kwanza | | Mwaka wa Pili | Idadi | Alama |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Muhula wa kwanza | Muhula wa Pili | | | |
| **Taaluma** | Majaribio | 1 | 1 | | 2 | 3 |
| | Kazi mradi | 1 | 1 | | 2 | 5 |
| | Mazoezi | 1 | 1 | | 2 | 2 |
| **Ufundishaji** | Majaribio | 1 | 1 | | 2 | 3 |
| | Mkoba wa Kazi | 1 | 1 | | | 5 |
| | Mazoezi ya kufundisha | 1 | 1 | | 2 | 2 |
| **Mtihani wa mwisho wa muhula** | Taaluma na Ufundishaji | 1 | 1 | | 2 | 15 |
| **Mazoezi ya Kufundisha** | 1. Maandalizi ya Ufundishaji<br>2.Ufundishaji darasani | | 1 | | 1 | 5 |
| **Mazoezi ya muda mrefu** | 1.Fomu za uchunguzi<br>2.Ufaraguzi wa zana<br>3.Mkoba wa Kazi | | | • | | 10 |
| **Jumla ya Alama za Upimaji Endelezi** | | | | | | **50** |
| **Mtihani wa Baraza la Mtihani wa Taifa** | | | | • | | **50** |
| **Jumla Alama za Upimaji Endelezi na Tamati** | | | | | | **100** |

**NB-**

i) Mazoezi ya darasani yawe na alama 20

BTP alama 5

Mitihani ya Mihula (miwili) alama 15

Mazoezi ya kufundisha muda mrefu 10

## 1.0 NAMBA

### 1.1 Vitendo vya Kuhesabu Vitu

**Muda: Saa 19**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza mbinu mbalimbali atakazotumia kuhesabu vitu

b) Kuaridhia hatua za kufuatwa kumfundisha mtoto kuhesabu vitu

c) Kubainisha mbinu na zana za kufundishia kuhesabu

d) Kuandaa andalio la somo la mfano la kuhesabu

e) Kufundisha somo la mfano la kuhesabu na kufanya tathmini

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji

ii) Onesho mbinu

iii) Nyimbo na michezo

iv) Mazoezi ya kufundisha

**Vifaa/zana za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Vitu mbalimbali vya kuhesabu katika mazingira

(ii) Fito na namba

(iii) Namba za mkwaruzo, kadi za namba, chati za namba

(iv) Shanga mraba

**Upimaji**

i) Jaribio

ii) Orodha hakiki

### 1.2 Vitendo vya Kusoma Namba

**Muda: saa 13**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza mbinu na hatua atakazotumia kumfundisha mtoto kusoma namba
b) Kutumia mbinu na hatua mbalimbali kusoma namba 1 hadi 10
c) Kubainisha mbinu na zana zitakazotumika katika kusoma namba
d) Kuandaa andalio la somo kuhusu kusoma namba
e) Kufanya ufundishaji kiduchu, tathmini ya somo alilofundisha na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Majadilino
ii) Onesho mbinu
iii) Nyimbo na michezo
iv) Ufundishaji kiduchu

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Namba za mkwaruzo
(ii) Michoro ya namba
(iii) Kadi/chati za namba

**Upimaji**

i) Insha
ii) Orodha hakiki

## 1.3 Vitendo vya Kuandika Namba

**Muda:** Saa 17

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza mbinu na hatua atakazotumia kumfundisha mtoto kuandika namba
b) Kubaini mbinu na zana za kufundishia kuandika namba
c) Kuandaa andalio la somo la kuandika namba
d) Kufundisha somo la mfano kuhusu kuandika namba

e) Kufanya tathmini ya ufundishaji na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Bungua bongo
ii) Majadilino
iii) Onesho mbinu

**Vifaa na Zana za Kufundishia/Kujifunzia**

i) Makunzi yanayopatikana katika mazingira
ii) Vibao vya kuandikia
iii) Kadi/chati za namba
iv) Namba za mkwaruzo

**Upimaji**

i) Majaribio
ii) Fomu ya uchunguzi

## 1.4 Vitendo vya Kuongeza na Kupunguza vitu

**Muda:** Saa 15

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza mbinu na hatua atakazotumia kumfundisha mtoto kuongeza na kupunguza vitu
b) Kuonyesha jinsi atakavyomfundisha mtoto kuongeza vitu kupata jumla isiyozidi 10 na kupunguza vitu kutoka 10 hadi 1
c) Kuandaa andalio la somo la kufundisha kuongeza na kupunguza vitu
d) Kufanya mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja shulu jirani
e) Kufanya tathmini ya ufundishaji na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Fikiri, jozisha shirikisha
ii) Onesho mbinu
iii) Nyimbo, hadithi, maigizo na michezo
iv) Mazoezi ya kufundisha

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Vitu halisi katika mazingira
ii) Kadi/chati za namba

**Upimaji**

i) Insha
ii) Orodha hakiki

## 2.0 FEDHA

### 2.1 Dhana ya Fedha

**Muda:** Saa 3

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza dhana ya fedha na mbinu atakazotumia kumfundisha mtoto kutambua fedha
b) Kutofautisha fedha za noti na sarafu za Tanzania
c) Kubaini mbinu na zana za kufundishia dhana ya fedha
d) Kuandaa andalio la somo la dhana ya fedha
e) Kufundisha somo la mfano kuhusu dhana ya fedha, kufanya tathmini na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Bungua bongo
ii) Majadiliano
iii) Onesho mbinu
iv) Mazoezi ya kufundisha

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Fedha za sarafu

(ii) Fedha za noti

iii) Picha/michoro ya fedha za sarafu na noti

**Upimaji**

i) Majaribio

ii) Orodha hakiki

## 2.2 Matumizi na Utunzaji wa fedha

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza matumizi na utunzaji wa fedha

b) Kufafanua mbinu mbalimbali za kutumia fedha kwa usahihi

c) Kuandaa somo kuhusu matumizi na utunzaji wa fedha

d) Kufanya ufundishaji kiduchu wa matumizi na utunzaji wa fedha

e) Kufanya tathmini na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Majadiliano

(ii) Maigizo

iii) Nyimbo, hadithi na michezo

iv) Mazoezi ya kufundisha

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Fedha

(ii) Picha zinazoonyesha uuzaji na ununuaji wa bidhaa

iii) Picha zinazoonyesha watu wakiweka/wakichukua fedha benki

**Upimaji**

i) Insha

ii) Orodha hakiki

## 3.0 VIPIMO SAHILI

### 3.1 Dhana ya vipimo

**Muda: Saa** 5

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza dhana ya vipimo, aina za vipimo na vifaa vya kupimia
b) Kupima vitu mbalimbali kwa usahihi
c) Kubaini mbinu na zana za kufundishia dhana ya vipimo
d) Kuandaa andalio la somo la dhana yavipimo
e) Kufundisha somo la mfano kuhusu dhana ya vipimo, kufanya tathmini na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Bungua bongo

ii) Majadiliano

iii) Mazoezi ya kufundisha

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

Vifaa mbalimbali vya kupimia

**Upimaji**

i) Majaribio

ii) Orodha hakiki

## 4.0 WAKATI

### 4.1 Majira ya Siku

**Muda**: Saa 5

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kutofautisha dhana ya giza na mwanga
b) Kubainisha mbinu zitakazomwezesha mtoto kutambua asubuhi, mchana, jioni na usiku
c) Kuandaa somo kuhusu majira ya siku
d) Kufanya ufundishaji kiduchu wa majira ya siku
e) Kufanya tathmini na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Bungua bongo
ii) Maigizo
iii) Majadiliano
iv) Ufundishaji kiduchu

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Tochi
(ii) Mpira
iii) Michoro katika manila
(v) Picha zinazoonyesha mchana na usiku

**Upimaji**

i) Insha
ii) Orodha hakiki

## 4.2 Siku katika Juma

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

(a) Kubainisha mambo yatakayomfanya mtoto kutambua siku za juma

b) Kueleza umuhimu wa kutambua siku za juma

c) Kuandaa somo kuhusu siku katika juma

d) Kufanya ufundishaji kiduchu wa siku katika juma

e) Kufanya tathmini na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Majadiliano

(ii) Igizo

iii) Nyimbo

iv) Ufundishaji kiduchu

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Ratiba ya vipindi

ii) Chati inayoonyesha siku za juma

(ii) Kalenda

**Upimaji**

i) Majaribio

ii) Orodha hakiki

## 5.0 MAUMBO

## 5.1 Dhana ya Maumbo

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

(a) Kueleza dhana ya maumbo na matumizi mbalimbali ya maumbo

(b) Kuchora maumbo mbalimbali

c) Kubaini mbinu na zana za kufundishia dhana ya maumbo

d) Kuandaa andalio la somo la dhana ya maumbo

e) Kufundisha somo la mfano kuhusu dhana ya maumbo, kufanya tathmini na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Majadiliano katika vikundi

ii) Onesho mbinu

iii Mazoezi ya kufundisha

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

(i) Vifaa vya kuchorea

(ii) Picha/michoro ya maumbo mbalimbali

iii) Kompyuta

**Upimaji**

(i) Majaribio

(ii) Fomu ya uchunguzi

## 5.2 Kutengeneza Mapambo

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubuni na kutengeneza mapambo na kuyapaka rangi

b) Kueleza umuhimu wa mapambo

c) Kubainisha mbinu na zana za kufundishia kutengeneza mapambo

d) Kuandaa somo la kutengeneza mapambo

e) Kufundisha somo la mfano kuhusu kutengeneza mapambo, kufanya tathmini na kutoa mrejesho

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

i) Onesho mbinu

ii) Majadilino katika vikundi

iii) Mazoezi ya kufundisha

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

i) Vifaa vya kutengenezea mapambo vinavyopatikana katika mazingira

(ii) Karatasi za rangi mbalimbali

(iii) Kalamu za rangi

(iv) Mkasi

**Upimaji**

(i) Majaribio

ii) Fomu ya uchunguzi

**REJEA**


1. Chowo H. T. (2007) *Elimu ya Awali Mwandani* wa mwalimu, Mture Education Publisher Ltd, Dar es Salaam.
2. Agakhan Educatioan service Tanzania (1990) *Mwongozo wa Mtaala ya Walimu wa Shule za Awali*, Dar es Salaam
3. Moyo P. (2007), Englsh for pre-School Oxford University press, Dar es Salaam.
4. National Institute of Technical Teachers Training and Research (2006) Instructional materals Development Chennal.
5. Taasisi ya Elimu Tanzania (2005). *Mwongozo wa ufundishaji Elimu ya Awali*, Dar es Salaam.
6. Taasisi ya Elimu Tanzania (2003). *Moduli ya somo la malezi ya elimu ya awali*. Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti DSM.
7. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1987). *Malezi na Elimu ya watoto wadogo* Dar es Salaam.
8. Wizara ya elimu na Utamaduni (1991). Mwongozo wa shule za Awali. Printfast publisher (T) Ltd Dar es Salaam.
9. Wizara ya Elimu na Utamaduni 2003: *Muhtasari wa mafunzo ya Ualimu, Ngazi ya Cheti mbinu za Kufundishia na kujifunzia Elimu Awali* Dar es Salaam.
10. Wizara ya Elimu na Utamaduni (2005):. *Muhtasari wa stadi za kazi kwa shule za msingi*.
11. Wizara ya Elima na Utamaduni (2005): *Muhtasari wa Elimu ya Awali kwa Shule za Awali* Dar es Salaam.
12. Wizara ya elimu na Utamaduni (2003): *Ufundishaji Unaozingatia Ujenzi wa Maana*. Ecoprint ltd Dar es Salaam.

# VITENDO VYA KUJIFUNZA SAYANSI

**Ujuzi**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili ngazi ya cheti Elimu ya Awali mwanachuo atakuwa amepata ujuzi wa:-

1. Kuwaelekeza watoto kutambua umuhimu wa usafi na utunzaji wa afya.
2. Kutambua mazingira yanayomzunguka mtoto na kuweza kuyatumia kwa makuzi na malezi bora ya mtoto.
3. Kutumia mbinu anuai kuwaelimisha watoto, wazazi na jamii juu ya magonjwa mbalimbali na jinsi ya kuyaepuka.
4. Kutumia mbinu anuai kumjengea mtoto stadi za uchunguzi na ugunduzi wa kisayansi.

**Malengo**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili ya ualimu ngazi ya cheti Elimu ya Awali mwanachuo aweze:

1. kutumia mbinu mbalimbali za kuwaelekeza watoto usafi na utunzaji wa afya.
2. kutumia maarifa na stadi za kumwelekeza mtoto mbinu anuai za uchunguzi na ugunduzi katika sayansi.
3. kubaini magonjwa na hatari zinazowakabili watoto ili aweze kuwaelimisha watoto, wazazi na jamii namna ya kuziepuka.

**Upimaji**

Mwanachuo atapimwa kwa mazoezi ya darasani, majaribio, kazi mradi, ufundishaji wa mazoezi (vitendo), mitihani ya mihula na mtihani wa mwisho.

Mtihani wa mwisho utakuwa na uzito wa 50%. Vipengele vingine vitakuwa na uzito wa jumla ya 50% kwa mtawanyo kama unavyoonenkana katika jedwali liufuatalo:

**Jedwali la Upimaji Endelevu na Tamati**

| Vipengele | Mbinu za Upimaji | Mwaka wa Kwanza | | Mwaka wa Pili | Idadi | Alama |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Muhula wa kwanza** | **Muhula wa Pili** | | | |
| **Taaluma** | Majaribio | 1 | 1 | | 2 | 3 |
| | Kazi mradi | 1 | 1 | | 2 | 5 |
| | Kazi za kila mwanachuo | 1 | 1 | | 2 | 2 |
| **Ufundishaji** | Majaribio | 1 | 1 | | 2 | 3 |
| | Mkoba wa Kazi | 1 | 1 | | | 5 |
| | Kazi za vitendo | 1 | 1 | | 2 | 2 |
| **Mtihani wa mwisho wa muhula** | Taaluma na Ufundishaji | 1 | 1 | | 2 | 15 |
| **Mazoezi ya Kufundisha** | 1. Maandalizi ya Ufundishaji<br>2.Ufundishaji darasani | | 1 | | 1 | 5 |
| **Mazoezi ya muda mrefu** | 1.Fomu za uchunguzi<br>2.Ufaraguzi wa zana<br>3.Mkoba wa Kazi | | | • | | 10 |
| **Jumla ya Alama za Upimaji Endelezi** | | | | | | **50** |
| **Mtihani wa Baraza la Mtihani wa Taifa** | | | | • | | **50** |
| **Jumla Alama za Upimaji Endelezi na Tamati** | | | | | | **100** |

**NB-**

i) Mazoezi ya darasani yawe na alama 20
BTP alama 5
Mitihani ya Mihula (miwili) alama 15
Mazoezi ya kufundisha muda mrefu 10

## 1.0 USAFI

### 1.1 Dhana ya Usafi

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza dhana ya usafi

b) Kufafanua madhara ya uchafu

c) Kubainisha mbinu na zana za kufundishia dhana ya usafi

d) Kuandaa somo la dhana ya usafi

